



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)**

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb: Na. HWC/L.20/03/VOL/X/76

20.10.2025

**MKURUGENZI MTENDAJI,
TANZANIA INVESTMENT AND SPECIAL ECONOMIC ZONES AUTHORITY (TISEZA),
S.L.P 938,
DAR ES SALAAM.**

**YAH: KIWANJA NAMBA 4 KITALU "18A" KATIKA ENEO LA CHAMAKWEZA
CHALINZE KWA MWEKEZAJI WEILONG COMPANY LIMITED.**

Tafadhali husika na, somo tajwa hapo juu.

Tunapenda kukutaarifu kuwa tarehe **16.10.2025** ofisi ilipokea barua kutoka kwa Kampuni tajwa hapo juu ikiomba kumilikishwa kiwanja tajwa ambayo imeonesha nia ya kuwekeza katika kijiji cha Chamakweza kitongoji cha Mbala ambapo kijiji kilipokea maombi ya kumilikishwa eneo lenye ukubwa wa ekari 25.

Mtendaji wa Kijiji alieleza kuwa Kampuni ya **WEILONG COMPANY LIMITED** ya **S.L.P 7788**, **DAR ES SALAAM**, hapa nikiirejea kama kampuni ya kigeni ambayo inawakilishwa na ndugu **Moses Leoni Kimaro** (Mtanzania ambaye ni mwanasheria wa kampuni tajwa) inaomba kumilikisha eneo lenye ukubwa wa **(89,455 mita za mraba)** kwa ajili ya cha **kiwanda cha kuchakata vifaa vya ujenzi**.

Kampuni ya **WEILONG COMPANY LIMITED** ilipata eneo hilo kutoka kwa Wananchi wazawa wapatao saba ambao ni **NANU ATHUMANI MACHAKU, HAMISI GABRIEL KAZIDI, RAIS SUMLEKI KWANGU, MUOGA PARIYA KASHIMA, BABU BABU PARIYA KASHIMA, JUMA RAIS SUMLEKI,** na **MANG'OMBE RAIS LEKINYOTI** ambao waliokubalina wasimamiwe na ndugu **NANU ATHUMANI MACHAKU** katika mauzo ya maeneo yao. Kampuni hiyo ililipa stahili za Wananchi hao kwa kuzingatia makubaliano yaliyowekwa kati ya wananchi na kampuni tajwa na baadaye kuwasilisha ombi la umilikishaji kwenye Halmashauri ya kijiji hicho.

Baada ya kampuni kukamilisha taratibu za kulipa stahili za wamiliki asili, maombi ya kumiliki ardhi hiyo yalijadiliwa na Halmashauri ya kijiji tarehe **19.08.2025** na mapendekezo ya kikao cha Halmashauri ya kijiji yaliwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji cha Chamakweza uliofanyika tarehe **19.8.2025** ambapo kwa mujibu wa **Sheria ya Ardhi ya kijiji sura ya**

114, kijiji kilipendekeza mwombaji apewe eneo hilo lenye ukubwa wa **25** ambapo mwekezaji atapaswa kufanya yafuatayo kwenye kijiji:

- (a) Kuchangia maendeleo katika kijiji hususani kujenga nyumba ya daktari (Zahanati ya Chamakweza)
- (b) Wakazi wa kijiji cha Chamakweza wapewe kipaombe cha ajira kwa kuzingatia sifa walizo nazo
- (c) Shughuli za uwekezaji zisichafue mazingira ya kijiji cha Chamakweza

Baada ya kupokea maombi hayo, timu ya wataalam ilifanya ukaguzi tarehe 12/09/2025 na tulibaini yafuatayo:

- (a) Uwepo wa eneo lenye ukubwa wa ekari 25 na kutokuwepo kwa malalamiko wakati wa ukaguzi na eneo halijafanyiwa maendelezo yoyote
- (b) Eneo limepangwa na kupimwa kwa matumizi ya kiwanda

Kwa sababu hizo, tunapenda kudhibitisha kuwa eneo hilo ni mali ta Kampuni ya WEILONG COMPANY LIMITED ambayo amenunua kutoka kwa Wananchi wazawa wapatao Saba waliosimamiwa na NANU ATHUMANI MACHAKU.

Pamoja na barua hii, nimeambatisha nyaraka zifuatazo:

- a) Mkataba wa mauziano
- b) Muhtasari Halmashauri ya kijiji na mkutano mkuu uliojadili na kuridhia maombi yaliyowasilishwa kwa mujibu wa Sheria
- c) Udhhibitisho wa uraia (pasi za kusafiria)
- d) Nyaraka za usajili wa kampuni

Naomba kuwasilisha kwa hatua zinazofuata za kuwapatia cheti uwekezaji.


Ramadhani Possi
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
CHALINZE



Nakala kwa:

WEILONG COMPANY LIMITED

S.L.P 7788,

DAR ES SALAAM (kwa taarifa na ufuatiliaji).

Mtendaji wa Kijiji Cha Chamakweza (kwa taarifa)